

TUFATE NJIA YA MSALABA



Tu fwa te Nji a ya -- Msa la --- ba



tu i fwa te mpa ka kal va ri o ---



tu si ma me po bi la ha ya Msa --- la



ba ---- Msa ---- la ba u po nya ro ho

Umekosa nini we Yesu
Kushtakiwa bure kwa Pilato
Wenye kustahili hukumu
Si wewe, si wewe Bwana, ni sisi.

Ole msalaba huo mzito
Apagazwa Mwana mpezi wa Mungu
Mwili waenea mateso
Alipa, alipa madhambi yetu.

Ona Muumba Mbigu na nchi,
Yupo chini mzigo wa mwelemea,
Na mtu kiumbe chake kwa ukali,
Ampiga, ampiga bila huruma.

Huko njiani we Maria,
Waonaje hali ya Mwanao,
Ni damu tupu na vidonda,
Machozi, machozi yamfumba macho.

Kwa Simoni heri ya kweli
Mimi pia Yesu nisaidie
Kuchukua mzigo wa ukombozi
Kuteswa, kuteswa pamoja nawe.

Uso wa Yesu Malaika
Betlehemu walikuabudu
Bahati yake, Veronika
Kupangusa, kupangusa Mfalme wa Mbingi.

Wakimvuta huku na huku
Wauaji wanamchokesha bure
Chini wantupa bado kwa nguvu
Aibu, Aibu yao milele.

Wanawake wa Israeli
Msilie kwa sababu hiyo
Muwalilie hao kwa dhambi
Upanga, upanga ni juu yao.

Mwokozi sasa ni ya tatu
Waanguka chini ya Msalaba
Katika dhambi za uregevu
Nijue, nijue kutubu hima.

Muje Malaika wa Mbingu,
Funikeni mwiliwe kwa huruma,
Vidonda vyake na utupu,
Askari, askari wamemvua.

Hapo mkristu ushike moyo
Bwana wako alazwa msalabani
Mara miguu na mikono
Yafungwa, yafungwa kwa misumari.

Yesu mpenzi nakuabudu
Msalabani unapohangaika
Nchi yatetemeka kwa hofu
Na jua, na jua linafifia.

Mama Maria Mtakatifu
Upokee maiti ya Mwanao
Tumemwua kwa dhambi zetu
Twatubu, twatubu kwake na kwako.

Pamoja nawe kaburini
Zika dhambi na ubaya wa moyo
Yesu tuwe wakristo kweli
Twakupa, twakupa sasa mapendo.

Katika roho yangu Bwana
Chora mateso niliyokutesa
Nisiyasahau madeni
Na kazi, na kazi ya kuokoka.